11 potahiriwa, akapokea ishara ya tohara, mu-
huri wa haki ya imani iliyo asipotahiriwa,
apate kuwa baba wao waaminio wasipotahi-
12 riwa, haki ikahesabike kwao; na baba wa to-
hara, wala si wao wenyi tohara tu, illa wafua-
tao nyayo za imani yake baba wetu Ibrahimu
13 wakati asipotahiriwa. Kwani ahadi kwa
Ibrahimu na kwa mzao wake, si kwa sheria,
atauritbi ulimwengu, illa kwa haki ya imani.
14 Kwani kama wale walio katika sheria wange-
rithi, imani ingebatilika, ahadi ingetanguka,
15 kwani ndiyo sheria ifanyayo hasira; pasipo-
kuwako sheria, hapana kukosa.

16 Kwa hiyo kwa imani, iwe kwa neema,
ahadi iwe imara kwa wazao wote, si kwa
wale wa torati tu, illa tena wale wa imani wa
17 Ibrahimu, aliye baba wetu wote. Kama
yalivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba
wa mataifa mengi. Mbele ya Muungu ali-
yemwamini, awafanyaye hayi waliokufa,
18 ayaitaye yasiyo kama yamekuwa. Aliye-
amini kwa tumaini pasipo tumaini, apate ku-
wa baba wa mataifa mengi, kama lililonen-
19 wa, Hivi litakuwa zao lako. Asiyethoofika



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

katika imani, hakujikumbuka mwili wake
kama umekwisha kufa, akiwa na miaka ka-
20 ma mia, wala ufu wa tumbo lake Sara, kwa
ahadi ya Muungu hakuwa na shaka atoe
kuamini, illa kwa kuamini akapata nguvu,
21 akimtukuza Muungu, akithubutika kama
22 aliyeahidi akaweza kufanya. Kwa hiyo ika-
hesibika kwake kuwa haki.
23 Hayakuandikwa kwa ajili yake tu, kama
24 imehesabika, illa kwa ajili yetu tena, tuta-
kaohesabikia tukimwamini aliyemfufua Isa
25 Bwana wetu katika wafu, aliyetolewa kwa
makosa yetu, akafufuka kwa kutufanyia
haki.
V. Bassi tukipewa haki kwa imani, tunayo
amani na Muungu kwa Bwana wetu Isa
2 Masiya, kwa huyo tumepata katika imani
kuifikia neema hii, tunayoisimamia, tukifu-
rahiwa na tumaini la utukufu wake Muungu.
3 Wala si hiyo tu, illa twafurahi katika shidda,
4 tukijua kama shidda hufanya uvumilivu, na
uvumilivu kuthubutika, na kuthubutika tu-
5 maini, nalo tumaini lisilotia haya, kwani u-
pendo wa Muungu umemiminika mioyoni



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

mwetu kwa Roho Mtakatifu tuliyopewa.
6 Tena Masiya, tukiwa sisi thaifu, kwa wa-
7 kati wake akafa kwao waovu. Kwani kwa
mtu wa haki mtu hafi illa kwa shidda, kwa
mtu mwema labuda na mtu atathubutu kufa.
8 Muungu akaonyesha upendo wake kwetu
kama, tukiwa sisi tumekosa, Masiya kwa sisi
alikufa.
9 Sembuse sasa tukipewa haki katika da-
mu yake tutaokoka naye katika hasira.
10 Kwani tulipokuwa maadui tukapatanishwa
na Muungu kwa kufa Mwana wake, sembu-
se tukipatanishwa tutaokoka kwa uzima
11 wake. Illa si hiyo tu, tumefurahishwa tena
katika Muungu kwa Bwana wetu Isa Masi-
ya kwa huyo tuliyempokelea upatanisho.
12 Hivi, kama kwa mtu mmoja thambi imeingia
ulimwenguni, na kwa thambi kufa, kufa ku-
kapita juu ya watu wote, kwa sababu wote
13 wamekosa, kwani hatta sheria kukosa kuli-
kuwako katika ulimwengu, illa kukosa ha-
14 ina maana pasipo sheria, kufa kukamiliki
tangu Adamu hatta Musa juu yao wasioko-
sa kwa ginsi ya thambi yake Adamu, aliye



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

namna yake atakayekuja.
15 Illa si kama anguko ni ukarimu. Ikiwa
kwa kuanguka mtu mmoja walio wengi wa-
mekufa, sembuse neema ya Muungu, nalo
alilolitoa katika neema ya mtu mmoja, Isa
Masiya, limezidi kwao walio wengi.
16 Wala si kama kwa mmoja aliyekosa hili
alitoalo, kwani hukumu ya mmoja kwa ku-
hukumia, ukarimu ni wa matelezo mengi
17 kwa kuwa na haki. Ikiwa katika kuteleza
mmoja kufa kumemiliki kwa mmoja, se-
mbuse wapokeao wingi wa neema, na ku-
pewa haki katika uzima, watamiliki kwa
18 mmoja, Isa Masiya. Kama tena kwa ku-
anguka mmoja kuhukumiwa kwa watu wote,
hivi na kwa haki ya mmoja kwa watu wote
19 kupewa haki ya uzima. Kwani kama kwa
kuasi mtu mmoja, walio wengi wamekuwa
na thambi, hivi na kwa kutii mtu mmoja
walio wengi wamekuwa na haki.
20 Sheria ikaingilia anguko liwe kubwa;
ukiwa kubwa anguko, neema ikazidi kuwa
21 nyingi, illi kama kukosa kumemiliki katika
kufa, hivi na neema imiliki kwa haki hatta



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

uzima wa milele kwa Isa Masiya Bwana
wetu.
VI. Tusemeje tena? Tufanye thambi illi nee-
2 ma izidi? Hasha. Walioifia thambi wapate-
3 je kuishi katika thambi? Hamjui kama
waliobatizwa kwa Masiya Isa, kwa kufa
4 kwake wakabatizwa. Kwani tumezikwa
pamoja naye kwa ubatizo kwa kufa, illi, ka-
ma Masiya alivyoondoka katika wafu kwa
utukufu wa Baba, naswi tutembee katika
5 upya wa uzima. Tukipandwa pamoja naye
katika mfano wa kufa kwake, tutakuwa
6 tena katika ule wa ufufuo wake. Tukijua
kama mtu wetu wa kwanza amesulibishwa
pamoja naye, mwili wa thambi uharibike,
7 tusitumike tena sisi na thambi. Kwani ali-
yekufa amekuwa huru katika thambi.
8 Tukifa pamoja naye Masiya twaamin
9 kama tutaishi pamoja naye, tukijua kama
Masiya akiondoka katika wafu, hafi tena,
10 kufa haku'mwezi tena. Alivyokufa, aliifia
thambi mara moja; alivyoishi, amwishia
11 Muungu. Hivi na ninyi jihesabuni wafu
kwa thambi, wahayi kwa Muungu katika



Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is

Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is
Masiya Isa.
12 Bassi thambi isitawale katika mwili wenu
13 ufao, kwa kuzitii tamaa zake, wala msifa-
nye viungo vyenu selaha za thulumu katika
thambi. Illakini mjifanyize kwa Muungu
kama wahayi katika kufa, na viungo vyenu
14 selaha za haki katika Muungu, kwani tha-
mbi haiwawezi, kwani hampo chini ya she-
ria, illa chini ya neema.
15 Nini tena ? Tutende thambi, kwa saba-
bu hatupo chini ya sheria illa chini ya nee-
16 ma ? Hasha. Hamjui kama yule mtakaye-
jifanyizia watumwa mmtii, mmekuwa wa-
tumwa wake mmtiaye, ikiwa wa thambi kwa
17 kufa, ikiwa wa kutii kwa haki ? Muungu
ashukuriwe, kama mlikuwa watumwa wa
thambi, mkafuata kwa moyo namna ya ma-
18 fundisho mliyoipokea, mkiwekwa huru ka-
tika thambi mkatumika katika haki.
19 Nasema kwa mwana Adamu kwa sababu
ya uthaifu wa mwili wenu. Kama mlivyo-
weka viungo vyenu kutumika na uchafu na
uovu kwa uovu, hivi sasa, mweke viungo
vyenu kutumika na haki kwa kusafishwa.

Cambridge University Library
www.lib.cam.ac.uk/is